tena, kikombe kinaakilisha nini? Jibu ni kwamba, sahani, kikombe haviakilishi chochote. Havina maana ya kiroho yo yote..

Katika Mdo.15 wengine walijaribu kulazimisha tohara juu ya kanisa. Walifundisha kwamba, mtu hawezi kuokolewa asipotahiriwa. Walikuwa wanaweka sheria pale ambapo Mungu alikuwa hajaweka. Walikuwa wanaweka kipimo cha ushirika kutokana na mawazo yao wenyewe. Siku hizi, ndugu wa kikombe kimoja wanafanya vile vile. Wanafunga mahali Mungu hajafunga. Wanaweka kipimo cha ushirika kutokana na mawazo yao wenyewe. Mwili wa Kristo unathamani sana ya kufanya hivyo. Tunachotakiwa kuwekea mkazo ni kwamba, makanisa yanakula meza ya Bwana katika kila siku ya kwanza ya Juma. Lakini tusifunge idadi ya vikombe vya mzao wa mzabibu, au idadi ya sahani za kuwekea mikate.

"Nakujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani." (Efeso 4:3) Idadi ya vikombe vyakutumia katika mzao wa mzabibu, visiendelee kutenganisha kanisa, wala hata kama hatukutani orofani jinsi walivyo kutana wao.

vikombe 12 kutokana chupa moja, na kunywa inaweza kusemekana kuwa wote wamekunywa chupa moja. Yesu alipochukuwa kikombe na kusema nyweni nyote, alimaanisha kunywa kilichokuwamo ndani ya kikombe au kunywa kikombe chenyewe? Hii ilikuwa ni lugha ya mfano inayojulikana kama Metanomi. Sahani moja au nyingi haivunji amri ya kula mkate. Sahani si muhimu; mkate unaakilisha mwili wa Kristo.

moja. Yesu alipochukuwa kikombe na kusema nyweni nyote, alimaanisha kunywa kilichokuwamo ndani ya kikombe au kunywa kikombe chenyewe? Hii ilikuwa ni lugha ya mfano inayojulikana kama Metanomi. Sahani moja au nyingi haivunji amri ya kula mkate. Sahani si muhimu; mkate unaakilisha mwili wa Kristo.

Hata ndivyo ilivyo kweli kuhusu mzao wa mzabibu. Kikombe kimoja au vingi havivunji amri ya kunywa nyote katika hiki. Chombo siyo muhimu, mzao wa mzabibu unaakilisha damu ya Kristo. Nina uliza

---

International Bible Teaching Ministries
P.O. Box 49494
Cookeville, TN. 38506

www.IBTM.org

# Kikombe Kimoja

Au

## Vikombe Vingi?

**Mbuni:**
**Ronald D. Gilbert**
**(One Cup- Kiswahili)**

Kwa habari zaidi, tuandikie:

Je, ni lazima kusanyiko la kanisa la Bwana wanapokunywa mzao wa mzabibu wakati wa chakula cha Bwana, watumie kikombe kimoja tu? Swali hili limesababisha mgawanyiko mkubwa katika kanisa la Bwana. Katika maandishi haya, tunakwenda kutafakari swali hili.

Wale wanaodai kuwa ni lazima kutumia kikombe kimoja kila mara kanisa linapokunywa mzao wa mzabibu,wanatoa mistari hii:

Mathayo 26:27- "Akatoa kikombe…."
Marko 14:23- "Akatoa kikombe….."
Luka 22:20- "Kikombe nacho vivyo.."
1Kor. 10:16 "Kikombe kile cha baraka…"
1Kor. 11:25 "…....Akakitoa kikombe….."
1Kor. 11:26 ".mkate huu na kukinyweya kikombe hiki..."
1Kor. 11:27 "……...kila aulaye mkate au kukinyweya kikombe…...."
1Kor. Kor.11:28 "……...aule mkate na kukinyweya kikombe…..."

Tunatakiwa kutumia kwa halali Maandiko Matakatifu (II Tim. 2:15). Katika vifungu kuhusu chakula cha Bwana, kuna vitu vinaozungumziwa katika lugha ya mfano. Tafakari pointi tatu zifuatazo na kujibu swali la tatu.

1. Mkate unaakilisha mwili wa Kristo katika chakula cha Bwana.
2. Mzao wa mzabibu unaakilisha damu ya Kristo.
3. Kikombe wanamoweka mzabibu kinaakilisha nini?

Je, kila sehemu ya mfano inafaa kufuatwa?
1. Katika Matendo ya Mitume 20:7-8 walikutana katika chumba cha (gorofani) Je, kanisa la leo linapaswa kufuata mfano huo?
2. Yesu alibatizwa katika mto Jordani, ni lazima na sisi kufuata mfano huo na kwenda kubatizwa katika Jordani?
3. Yesu alibatizwa katika mto, je, tunaweza kubatizwa katika kisima cha ndani ya jengo au katika bahari?

Wale wanaodai matumizi ya kikombe kimoja tu katika chakula cha Bwana , wanadai hivyo kwa kusema kuwa wanafuata mfano wa Yesu. Wanasema kutumia zaidi ya

Kikombe kimoja ni kupita yale yanayozungumziwa na Biblia. Wanasema ya kwamba, hakuna mamlaka ya Biblia yanayotoa matumizi ya kikombe kimoja. Wanauliza, wapi kifungu kinachaagiza matumizi ya zaidi ya kikombe kimoja? Wanasema, ukitumia zaidi ya kikombe kimoja utakuwa umepita mamlaka ya Biblia na kwa hiyo ni dhambi. Biblia inatuagiza kwa njia ya amri, mfano, usemi wa moja kwa moja, au kwa kile kinacho endeleza amri. Wale wanaong'ang'ania matumizi ya kikombe kimoja tu katika chakula cha Bwana, wanauliza swali, "Wapi amri, mfano, au msemo wa moja kwa moja unaotuagiza kutumia vikombe vingi katika chakula cha Bwana? Wanasahau kuhusu kile kinacho endeleza amri (kutusaidia) Hawana tatizo kuamru kujengwa kwa jengo la kanisa, au viti vya kukalia katika lile jengo, vitabu vya nyimbo, sahani zakuwekea mkate wa chakula cha Bwana na hata kuwa na zaidi ya mkate mmoja. Hayo yote wanayaamru kwa kuona itaendeleza amri (kusaidia) Wanatakiwa wawe watu walio namsimamo na kile wanachokidai. Ikiwa mambo hayo yote wanayaamru kwa kuona yanafaa, na hata ndivyo ilivyo matumizi ya vikombe vingi.

Sasa tafakari matumizi ya sahani za kuwekea mikate. Wapi fungu la maandiko linaloamrisha matumizi ya sahani moja au mbili ya kuwekea mikate? Watu hawa wanatumia sahani mbili au zaidi, bila kuwa na mamlaka yanayowaruhusu kufanya hivyo. Unaona, wanafahamu kwamba usemi, "mkate" mmoja una maana kuwa wote wanashiriki mkate. Wanafahamu kuwa, idadi ya sahani haibadilishi chochote, wote wanashiriki mkate mmoja. Kuna mamlaka ya Biblia iliyo sawa sawa na ile ya kuwa na zaidi ya kikombe kimoja.kwa njia inayofanana na mamlaka ya kuwa na sahani zaidi ya moja ya mkate. Chombo siyo muhimu, kilichomuhimu ni mzao wa mzabibu na mkate. Kikombe ni chombo cha kuendeleza amri ya kutumia mzao wa mzabibu vile vile sahani nayo ni msaada katika amri ya kula mkate. Idadi ya vikombe au sahani haijaelezewa.

Maswali kwa wale wanashikilia kutumia kikombe kimoja cha mzao wa mzabibu tu:

1. Endapo mkate mmoja waliokuwa wakiumega ukavunjika katika vipande kadha kwa bahati mbaya, je,washiriki wengine wakiutumia ule uliovunjika kabla wao wenyewe kuumega, watakuwa wameshiriki kimaandiko? Hii inasemekana kwa sababu Biblia inasema, Yesu alichukuwa "mkate" na siyo "mikate."
2. Ikiwa wakati wa kupitisha mzao wa mzabibu katika kusanyiko, ajali inatokea, kikombe kinanguka nakuvunjika, na kilichomo kumwagika, washiriki waliobaki watahudumiwaje kimaandiko?
3. Paulo katika 1 Wakorintho 10:16 alisema kwamba Wakristo waliokuwa Korintho na Uefeso kwa pamoja walibariki "kikombe", kama ni hivyo, usemi "kikombe" hapa una maanisha vikombe viwili, kimoja Efeso na kingine Korintho. Ikichuliwa hivyo, basi, neno kikombe kinaweza kumaanisha vingi.
4. Na aliposema kuwa wote walishiriki mkate mmoja, je, hakuwa na maana ya vipande vya mikate miwili, mmoja ukiwa Korintho na mwingine Efeso?

**Tafakari kuhusu kisima cha Yakobo** katika Yohana 4:12. "Je wewe umkubwa kuliko Baba yetu Yakobo, aliyetupa kisima hiki, naye mwenyewe akanywa yake, na wanawe pia na wanyama yake"? Je, hii ina maana ya kuwa kila mmoja alikuwa akiweka mdomo wake juu ya kisima na kunywa? Wote walikunywa kutoka hicho kisima kimoja lakini wote hawakutumia chombo kimoja.

**Tafakari kuhusu meza**. Luka 22:30 anasema, " mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu….." Na katika Luka 22:21 Yesu alisema, "Walakini, tazama, mkono wake anyenisaliti upo hapa pamoja nami mezani," Je hii inatufunga kwamba lazima tuwe na meza? Hatuwezi kuweka meza ya Bwana hata kwenye kiti cha kukalia?

Je, watu 12 wanaweza kunywa chupa moja kwa kutumia vikombe 12? Ndiyo. Siyo lazima kila mmoja weke mdomo wake kwenye chupa ndipo wawe wamekunywa chupa moja. Tukimwaga vikombe 12 kutokana chupa moja, na kunywa inaweza kusemekana kuwa wote wamekunywa chupa